Toleo la 4 - 2015

Ukurasa-------1

NGUVU yetu

"Making a real difference in lives"

UTANGULIZI

TUSONGE ni shirika la maendeleo ya jamii linalofanya kazi za kuwezesha jamii za pembezoni hususani wanawake na vijana kujikwamua kiuchumi na pia linatoa elimu ya Haki za Binadamu katika mkoa wa Kilimanjaro. Jamii ambazo TUSONGE inafanya nazo kazi zimeonekana kuwa na rasilimali za kutosha ambapo ikiwa zitatumika vizuri changamoto mbali mbali zinaweza kutatuliwa. TUSONGE imethamini jamii hizo kwa kuwapatia elimu ya ujasiriamali ili kuweza kutambua fursa zilizopo katika jamii.

Januari hadi Machi 2015, TUSONGE imeweza kutoa Elimu ya Ujasiriamali katika kata ya Msaranga ndani ya vikundi vinne ambapo kila kikundi kina jumla ya wanachama thelathini. Lengo kuu la elimu iliyotolewa ni kuwezesha jamii kuondokana na umaskini uliokithiri. Hadi kufikia sasa wanajamii waliopata mafunzo hayo wanaendelea kuyafanyia kazi kwa vitendo ili wapate mabadiliko yatakayoonekana.

Wakati mafunzo ya ujasiriamali yakiendelea kata ya Msaranga, kata ya Ivaeny na Biriri ndani ya wilaya ya SIHA na kata ya Majengo Manispaa ya Moshi kazi ya ufuatiliaji iliendelea lengo likiwa ni kushuhudia mabadiliko yaliyojitokeza kwa wanajamii waliopata mafunzo kwa miaka iliyopita.

Shirika la TUSONGE limeweza kupima mabadiliko yanayojitokeza kwa jamii kwa njia mbalimbali. Njia moja wapo ni shuhuda, picha, mahojiano ya moja kwa moja, vikao vya timu ya ufuatiliaji shirikishi na mikutano ya wanavikundi wakati wa ununuzi wa hisa. Hali ya ukusanyaji wa taarifa kwa kutumia njia hizo imeibua hamasa kwa wanufaikaji wa mradi huo kwa kujitahidi kufanya kazi kwa bidii ili kuweza kushirikisha maendeleo yao baada ya kujiunga na Mradi wa TUSONGE. Kata za Majengo na Miembeni kwa sasa wapo katika hatua za kuanzisha mradi wa Pamoja wa kufungua **DUKA LA VIFAA VYA UJENZI.** Hii ni baada ya kujiunga vikundi vyote vilivyopata mafunzo kutoka TUSONGE na kuanzisha Mtandao wao wa kufanya kazi kwa pamoja unaojulikana kama Mtandao wa Wajasiriamali Moshi (MTAWAMO) ambao una jumla ya wanachama 180. MTAWAMO una katiba yao inayowaongoza. MTAWAMO imeandikishwa rasmi katika Manispaa ya Moshi na Namba ya Utambulisho ni **MMC/CBO/221/2012**. Wanachama wa MTAWAMO ni wale waliokwisha kufuzu mafunzo ya TUSONGE na kukubali sasa kujiunga ili kuweza kuleta mabadiliko makubwa zaidi katika jamii zao. Hadi kufikia hivi sasa tunategemea kuwa na wanachama kutoka vikundi vitatu vya Msaranga. Hii itasaidia Mtandao kusonga mbele kutokana na uongozi imara. TUSONGE inaendelea kutoa ushauri kwenye MTAWAMO ili kuhakikisha mradi uliokusudiwa na wanachama hao umesimama na kufanya kazi. TUSONGE inawajengea uwezo kuendelea kudai haki ya elimu endelevu toka serikalini, mikopo midogo midogo na kuwaunganisha na wadau wengine ili kutandaa kibiashara na kupata mikopo zaidi.

Shirika la TUSONGE limeweza kuhojiana na walengwa mbalimbali katika Kata za Msaranga na Majengo ndani ya Manispaa ya Moshi, Ivaeny na Biriri wilaya ya Siha.

TUSONGE kwa kuwa inaheshimu dhana ya ushirikishwaji inapenda kukualika wewe kama msomaji wa gazeti hili kuungana katika kuhakikisha malengo ya jamii yanatimizwa kwa kutoa ushauri na michango mbalimbali ili kuhakikisha mradi unakuwa endelevu.

Ahsanteni

Aginatha Rutazaa

MKURUGENZI MTENDAJI

Kwa maelezo /ushauri tuma kwa:
TUSONGE COMMUNITY DEVELOPMENT ORGANIZATION
P.O. Box 1326 – MOSHI
Simu: 0272754158
0762-303755
E-mail: tusonge@tusonge.org
Website: www.tusonge.org

Walengwa wa Tusonge waliokwisha kupata mafunzo wakitoa shuhuda zao kama ifuatavyo:

Agness Kambi, Nina umri wa miaka 52, ni mama mwenye watoto 5, ninatokea kata ya Majengo Kikundi namba 2, nilifanikiwa kujiunga na VICOBA mwaka 2011. Kabla ya kujiunga na Tusonge kwa kweli hali yangu ya kimaisha haikuwa nzuri hata kidogo. Hii ni kwa sababu sikuwa na uelewa wowote kuhusu ujasiriamali, nilikuwa sina biashara yenye msimamo kwani nilikuwa ninauza chipsi na mashuka bila kuona faida yoyote, nilikuwa nikikopa fedha za biashara sehemu nyingi hivyo ilinipa shida sana wakati wa marejesho. Baada ya TUSONGE kutoa elimu mbali mbali Kata ya Majengo maisha yangu na familia yamebadilika kwa kiasi kikubwa. Elimu iliyotolewa ni Ujasiriamali, UKIMWI, Uongozi, Elimu ya utunzaji wa kumbukumbu na mahesabu, Haki za binadamu na Jinsia na Ushawishi na Utetezi. Elimu iliyotolewa imenisaidia sana kukabiliana na changamoto mbalimbali - nimeweza kuacha kukopa mikopo mingi na kubaki na kikundi cha TUSONGE tu, nimeweza kufanya biashara zenye faida na ubora zaidi, nimeweza kujiongezea kipato na kutunza fedha kwa uangalifu.

Kata ya Majengo nimefanyika baraka sana baada ya kupata Elimu ya UKIMWI na Lishe kutoka TUSONGE kwani nimeweza kutoa Elimu ya UKIMWI kwa jamii na kwa watu wanaoishi na VVU. Mimi binafsi nimekuwa nikipima afya yangu mara kwa mara bila hofu.

Elimu ya uongozi imenifanya kujiamini na kumiliki biashara yangu mwenyewe, kwani hivi sasa ninamiliki salon na bodaboda mbili, sambamba na hayo wanachama waliojiunga na MTAWAMO kwa kuona ujasiri nilionao wameweza kunichagua kuwa Katibu wa Mtandao huo, nimeweza kuwa Mjumbe wa Serikali za Mitaa kwa muda miaka 15 lakini kwa sasa nimeamua kupumzika kutokana na majukumu mengi ya Familia. Nimeona mabadiliko makubwa baada ya Mafunzo ya TUSONGE kwa sababu Mtaji wa biashara yangu umekuwa kutoka 60,000/= mwaka 2011 hadi hivi sasa 1,500,000/= kipato changu kimeongezeka kutoka 1,500/= hadi 10,000/= kwa siku. Nimeweza kununua pikipiki 2 na kufungua salon ya wanawake na pia nimeweza kuajiri watu wawili kwenye biashara zangu na ninawalipa mishahara bila usumbufu.

Elimu ya Ujasiriamali niliyopata toka Tusonge imeniwezesha kufungua salon

Aishi Maimu. Nina miaka 30, nimeolewa, nina watoto watatu. Ni mwanachama wa kikundi namba 3 Ivaeny. Nina jambo la kuwashirikisha ambalo kwa kweli ni furaha kutoka ndani ya moyo wangu. Mradi huu wa TUSONGE umekuwa mkombozi hasa kwa wanawake wa vijijini ambao wamekuwa wakijishughulisha na kazi za nyumbani kama vile kupika, kufua na usafi. Tangu mradi huu ulipoanza mwaka 2014 katika Kata yetu ya Ivaeny wanawake wengi wamenufaika. Hii ni kwa sababu kabla ya kupata mafunzo ya ujasiriamali akili yangu ilikuwa imefungwa na kunifanya kudumaa kibiashara. Sikuweza kuwa na mawazo ya kukuza biashara yangu zaidi ya ile ndogo niliyokuwa nayo.

Nilikuwa nafuga kuku wa kienyeji na mayai kidogo. Baada ya kujiunga na mradi wa TUSONGE, nimefanikiwa kupata elimu ya ujasiriamali ambapo tuliweza kufundishwa mambo mbali mbali ikiwemo wazo la biashara. Tuliweza pia kununua hisa kama tulivyofundishwa ndani ya vikundi. Mtaji wangu uliongezeka kutoka 20,000/=hadi shilingi 200,000/= kwa sasa nimeweza kuongeza vifaranga vya kuku wa Malawi nikavikuza. Kuku waliendelea kukua vizuri na kutaga mayai kwa wingi. Hadi kufikia hivi sasa nimefanikiwa kujulikana katika wilaya nzima ya SIHA kwa kuuza kuku wa aina ya Malawi kwa wateja tofauti tofauti. Ninawauza wakiwa vifaranga wadogo na kisha wanaenda kufugwa na kukuzwa. Pia nimeweza kuuza mayai ya kuku hawa ambapo dazeni moja ninauza kwa shilingi 15,000/= faida ninayoipata imeniwezesha kupata ada ya shule ya watoto wangu, kununua dawa za kuku, chakula na chanjo. Mbali na biashara ya kuku nimeweza kuvundika ngozi za ng'ombe na mbuzi na kuuza kwa jumla na rejareja. Hii ni baada ya mtaji wangu kuongezeka.

Aishi Maimu akionyesha namna anavyohifadhi ngozi za wanyama kabla ya kuzitengeneza chini akionyesha mpango wake wa biashara kwa Afisa ufuatiliaji wa Tusonge baada ya kupata mafunzo ya Ujasiriamali toka TUSONGE

Happyness Amani, Nina umri wa miaka 42 ni mjasiriamali Mtaa wa Rauya Kata ya Msaranga, ni mwanakikundi namba 3 Rauya. Kabla ya kujiunga na TUSONGE nilikuwa nikikumbana na changamoto mbali mbali katika biashara yangu kwani sikuwa na elimu ya ujasiriamali, sikujua namna ya kutofautisha faida na hasara, kipato cha biashara yangu kilikuwa kidogo kwa siku nilikuwa napata faida ya Shilingi 10,000/=, mtaji wangu ulikuwa shilingi 200,000/= tu, nilikuwa siweki kumbukumbu za biashara yangu hata kidogo, hii ilinifanya kusahau wadeni wangu na kusababisha hasara kwenye biashara yangu.

Niliweza kukabiliana na changamoto hizo baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali kutoka TUSONGE ambapo nilifundishwa namna ya kupata faida, nimefahamu umuhimu wa kununua bidhaa na kutunza risiti. Nimeweza kupata mabadiliko mbalimbali kwani mtaji wangu umekuwa kutoka 200,000/= hadi 1,000,000/= kipato kwa siku kimeongezeka kutoka 10,000/= hadi 30,000/= kwa siku nilikuwa nikifanya biashara ndogo ya duka hadi hivi sasa nimeongeza biashara ya Mamantilie, nimeweza kuajiri mtu mmoja, ninashirikishwa katika maamuzi ya familia tofauti na miaka iliyopita kutokana na hali duni niliyokuwa nayo sikuwa nashirikishwa lakini leo ninashirikishwa kikamilifu. Nimeweza kuvuta umeme kwenye nyumba yangu na bado nina maono ya kuongeza biashara yangu kwa kufuga kuku na nguruwe.

Dorothy Shoo, ni mama nimeolewa, nina watoto wa tatu, nina umri wa miaka 45. Ni mwanachama wa kikundi namba 3 Ivaeny, ninapenda kushukuru shirika la TUSONGE kwa kutupa nyavu ili tukavue samaki. Kwa kweli samaki tumeshaanza kuwavua kutokana na Elimu ya ujasiriamali nilioipata.

Elimu imenijenga na kunipa ujasiri wa kuthubutu kwani mwanzoni nilikuwa sijui nianzie wapi, lakini sasa najua pa kuanzia biashara, natambua faida na hasara kwa kupitia utunzaji wa kumbukumbu zangu. Nilianza kwa kuuza ndizi soko la Sanya Juu na sikuwa na biashara nyingine yoyote. Baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali na kuyafanyia kazi nimeanza kuona mabadiliko, mwanzo nilikuwa na mtaji wa shilingi 50,000/= kwa sasa mtaji wangu ni shilingi 200,000/= nimeanza kuona biashara yangu ikipanuka kutokana na utunzaji mzuri wa kumbukumbu. Hivyo niliweza kupata faida na kupanua biashara yangu.

Nilianza kuuza ndizi, nikaweza kuongeza maharage, mahindi ambayo nauzia nyumbani kwangu na pia elimu imeniwezesha kuwa mbunifu na sasa ninapamba kumbi za sherehe mbali mbali katika Kata ya Ivaeny. Nanunua jora moja la vitambaa vyenye rangi tofauti Kwa shilling 50,000/=, ninapamba kumbi kwa kiasi cha shilingi 150,000/= napenda kukukaribisha msomaji pale utakapohitaji huduma ya upambaji nipo kwa ajili ya kukusaidia. Namba yangu ya simu ni 0767-427986.

Moja ya Ukumbi aliopamba Dorothy Shoo

Joyce Owenya, nina umri wa miaka 42, ni mjane wa watoto watatu, ni mwanachama wa kikundi namba 3 Msaranga. Kama si TUSONGE sijui ningekuwa wapi, nakumbuka sikuwahi kuwaza kama ningeweza kujenga nyumba yangu mwenyewe kwani nyumba niliyokuwa nayo nilipata urithi kutoka kwa mama yangu mzazi, nimeishi kwenye nyumba hiyo kwa muda mrefu sana, baada ya kupata mafunzo ya ujasiriamali kutoka TUSONGE nimeweza kuona mabadiliko makubwa hii ni pamoja na mtaji wangu kukua kutoka shilingi 50,000/= hadi 1,000,000/=, kipato changu kwa siku kimeongezeka kutoka 5,000/= hadi 10,000/=. Baada ya ongezeko hilo nimeweza kukuza biashara yangu kutoka kilimo cha mpunga hadi molasses ambayo ninauzia nyumbani kwangu. Nimeweza kusomesha watoto wangu shule zenye mchepuo wa kiingereza, nimeweza kusaidia mtoto mmoja anayeishi katika mazingira magumu kwa kumpatia mahitaji yake sawa na watoto wangu, nimeweza kuongeza vyumba vinne vya wapangaji na sasa ninaendelea na ujenzi wa nyumba yangu ya kuishi ya kisasa.

Shirika la TUSONGE limeweza kupanua wigo wake kwa kuwashirikisha watu wanaoishi na ulemavu katika kutoa elimu. Kata ya Msaranga kipindi cha Januari hadi Machi vikundi vinne vilivyopata mafunzo ya ujasiriamali miongoni mwao wapo watu wanaoishi na ulemavu. Ulemavu huo ni kutokuona vizuri na hii imewapa shida na kuwafanya waogope na kujihisi wanyonge ndani ya jamii, hivyo basi TUSONGE imejaribu kutumia mbinu mbali mbali za ufundishaji ili watu wasioona waweze kushiriki kikamilifu bila kukosa. Kwa mfano TUSONGE imeweza kutumia njia za makundi ambapo watu hao wameweza kushiriki kutoa mawazo yao, pia njia za kunyoosha kidole katika kujibu maswali zimesaidia watu hao kutoa mawazo yao, njia za picha na kuwasomea maana ya picha hizo zimesaidia pia ushiriki wao. Wakati mwingine TUSONGE imeweza kuwatembelea watu hao na kufanya mahojiano ya kina ili waweze kuwa huru kwa kutoa changamoto wanazokumbana nazo katika biasahara zao.

Mmoja wao anaitwa Silvia biashara yake ni mamantilie, baada ya kupata mafunzo ya TUSONGE ameweza kufunguka kiakili na kujikubali, ameweza kuchangia mawazo kuhusu maendeleo ya kikundi na pia ameweza kuwa na furaha wakati akifanya biashara yake, ameweza kushirikisha malengo yake ya baadaye na pia amefurahi sana kwa ukaribu anaoupata kutoka TUSONGE.

***Silvia Maro**, nimeolewa Nina umri WA miaka 40, Ni mama mwenye watoto watatu, kabla sijajiunga Na mradi WA TUSONGE hali yangu ya kiuchumi ilikuwa sio nzuri, kwani nilikuwa na nyumba moja ya kulala yenye vyumba vitatu tu. Mtaji wangu ulikuwa mdogo sana kiasi cha shilingi 10,000/=, kipato changu kwa siku kilikuwa ni shilingi 2,500/= tu. Ambapo nilikuwa nikitumia fedha hiyo kwenye mahitaji ya nyumbani na bado ilikuwa haitoshi, baada ya kujiunga na mradi wa TUSONGE na kupata mafunzo ya ujasiriamali, mtaji wangu kwa sasa umekuwa kutoka 10,000/= hadi 500,000/= na kipato changu kwa siku kimeongezeka kutoka shilingi 2,500/= hadi 15,000/= nimeweza kujenga nyumba bora ya vyumba vitano, na vyumba vinne kwa ajili ya wapangaji. Maisha yangu na familia yameboreka kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kuweza kupata mlo mzuri mara 3 kwa siku, na kulipa ada ya shule ya watoto bila usumbufu.*

Mbali na kuwa mwanachama wa kawaida ndani ya kikundi, pia ni miongoni mwa wafuatiliaji shirikishi (PM & E) ndani ya jamii, nimekuwa nikifanya kazi hii kwa muda mrefu na bado ninaendelea nayo. Nimeweza kuona namna TUSONGE inavyofanya kazi zake kwa kushirikisha jamii. Hii imepelekea hali ya jamii kuwepo na jicho la ziada la kuona mabadiliko yanayojitokeaza katika jamii hasa kwa wakina mama kutokana na elimu iliyotolewa na TUSONGE. Pia mbali na mafanikio yaliyojitokeza kuna baadhi ya changamoto ambazo wanawake wachache wanakutana nazo. Kwa mfano wakati wakichukua mkopo waume zao wamekuwa wakichukua fedha hizo na kujikuta kwenye ulevi. Hii imekuwa ikileta shida wakati wa kurejesha, pia wanawake wengine wamekuwa wakichukua mikopo kwa siri ili waume zao wasijue. Wanawake wengi wameweza kukabiliana na changamoto hii kutokana na kuwa na uwezo wa kutetea haki zao. Hii imetokana na elimu ya haki za binadamu na jinsia iliyotolewa na shirika la TUSONGE.

Silvia Maro akielezea Elimu aliyopata TUSONGE imewafanya wanawake kuwa chachu ya mabadiliko katika familia zao na Kata ya Msaranga kwa ujumla

MAFANIKIO

- TUSONGE imefanikiwa kuanzisha mradi wa haki za watoto na vijana katika kata ya Ivaeny na Biriri ndani ya wilaya ya SIHA, Msaranga katika Manispaa ya Moshi. Lengo la mradi huu ni kuwajengea uwezo watoto na vijana katika kutetea haki zao za msingi ili kuheshimu usawa katika maswala ya Kiuchumi, kiuongozi na maamuzi katika jamii. Mradi huu una mahusiano makubwa na mradi wa Tusonge Unaotoa elimu ya uchumi na uongozi ndani ya jamii. Hii ni kwa sababu jamii inaweza kuwa na uchumi mzuri lakini ikakosa uelewa wa haki za watoto na vijana.

- TUSONGE imefanikiwa kugundua baadhi ya wanawake wenye mahitaji maalum kama vile wanaoishi na ulemavu wa kutokuona vizuri na kuwasaidia kupata haki zao.

- Shirika limeweza kuwa na mikakati ya kuwasaidia watu hao kama vile kutumia mbinu wezeshi za kufundisha elimu ya ujasiriamali na pia kuwatembelea katika biashara zao kwa ajili ya kutoa ushauri zaidi.

- Mbali na hivyo TUSONGE imeweza kuwasaidia wanufaikaji kutengeneza katiba inayowaongoza ndani ya vikundi. Wameweza kununua hisa mara moja kwa wiki kulingana na jinsi walivyojipangia wao wenyewe. Hivyo wananunua hisa ndani ya mwaka mmoja baada ya hapo wanavunja mzunguko na kugawana faida kwa kila mwanachama kulingana na jinsi walivyokopa. Siku hii ya kuvunja mzunguko wanachama wanaandaa risala inayoonyesha hali ya mwanzo ya kikundi kilipoanza mpaka kufikia sasa, pia wanaonyesha idadi ya fedha walizokusanya mwaka mzima ikiwa ni pamoja na hisa, mfuko wa jamii, pamoja na faini. Baada ya kuvunja mzunguko wanachama wanaanza mwaka mwingine kwa kukopeshana wao wenyewe kama ilivyokuwa awali.

Wanachama wa kikundi cha vijana wakitoa zawadi kwa Mkurugenzi wa Tusonge Mama Aginatha Rutazaa kwa mafanikio waliyoyapata

YALIYOJIRI KWENYE JAMII ZA TUSONGE MWEZI MEI HADI JUNI 2015

Tarehe 8 hadi tarehe 12 mwezi wa sita mwaka 2015 shirika la TUSONGE lilipata bahati ya kutembelewa na kufanyiwa tathimini kutoka kwa wafadhili wa mradi (mkate wa dunia). Tathimini hii ilifanyika ndani ya jamii tatu zilizopo mkoa wa Kilimanjaro sehemu ambapo mradi upo yaani; Kata za Msaranga na Majengo Manispaa ya Moshi, Ivaeny na Biriri zilizopo wilaya ya SIHA.

Shirika la TUSONGE linasema limepata bahati ya kufanyiwa tathimini kwa sababu, serikali ya ujerumani katika nchi zinazofadhiliwa hususani miradi ya kiuchumi ni jumla ya nchi 30 Barani Africa, kati ya nchi hizo zote walivutiwa sana na namna shirika la TUSONGE linavyofanya kazi ya kutoa elimu kwa jamii na kisha mabadiliko chanya kutokea kwa wanufaikaji wa mradi huo.

Lengo kuu la tathimini hiyo ni kujua maendeleo ya mradi huo kuanzia ulipoanza utekelezaji wake mwaka 2011 hadi kufikia hiv sasa mwaka 2015.
Kuweza pia kupata maoni toka TUSONGE kwa kuwa Mkate kwa dunia sasa wapo katika mchakato wa kutengeneza Mkakati mpya na wakahitaji wabia wao watoe maoni. TUSONGE iliwakilisha miradi ya Tanzania.

Matokeo ya awali ya tathimini yalikuwa kama ifuatavyo:
Wajasiriamali wadogo wadogo wameshauriwa kufanya biashara kama timu ili kuwa na maendeleo endelevu. Hii ni kutokana na mpango mkakati wa shirika la TUSONGE wa miaka mitano 2014-2018 unaoonyesha umuhimu wa kufanya biashara kwa njia ya sekta kama vile duka, mitumba, usafiri, kilimo na chakula. Mtathimini aliweza kukutana na wanufaikaji hao na kuwasikiliza kuhusu maoni yao ya baadae ambapo wengi wao walipendekeza kufanya biashara zinazofanana kwa njia ya Sekta ili kuongeza mguso na pia mabadiliko zaidi ndani ya jmaii zetu.

Kutumia fursa toka serikalini baada ya TUSONGE kuondoka kwenye jamii kama kupatiwa elimu mbalimbali za ujasiraimali kutoka ngazi ya serikali, secta binafsi, mashirika yanayotoa mafunzo ya ujasiriamali na ufundi kama vile SIDO na VETA.

Pia wataweza kupata fursa ya kutembelea siku za maazimisho ya kibiashara kama vile siku ya wakulima nane nane, siku ya sabasaba na maonyesho mengine. Hii itatumika kama fursa ya wajasiriamali kujifunza mbinu za biashara hususani kuongeza thamani ya bidhaa. Sambamba na hayo wajasiriamali watapata fursa ya kupata ruzuku kutoka serikalini pamoja na kupanua wigo wa kuisaidia jamii kwa mapana zaidi. Kama vile kusaidia yatima na watu wanaoishi na ulemavu

Mtathimini kutoka Ujerumani akikaribishwa Kwa furaha na kikundi cha vijana Wilaya ya Siha na kulia akikagua duka la Mjasiriamali aliyepata mafunzo toka TUSONGE

MRADI WA ELIMU YA HAKI ZA BINADAMU

Lengo la mradi
Kujenga jamii salama na zenye usawa zaidi ambapo wadau wakuu ikiwemo wanawake, watoto na vijana, wanashiriki na kuchukua nafasi za uongozi ili kukuza demokrasia na kuhakikisha haki za binadamu kuheshimiwa na kulindwa zaidi.

Mradi umefadhiliwa na Idara ya Mahusiano ya Kigeni, Biashara na Maendeleo toka nchini Canada kwa kupitia shirika la kimataifa linalotoa elimu ya haki za binadamu liiitwalo Equitas

Malengo:

- **Kuwajengea uwezo watoto na vijana** toka jamii lengwa kuongoza jitihada za jamii zinazolenga kupunguza ukatili, zinazokuza usawa wa kijinsia, na kuhakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa zaidi.

- **Kuongeza ushirikishwaji zaidi** wa wasichana, wavulana, wasichana wadogo, wavulana wadogo haswa kutoka makundi ya pembezoni katika maendeleo ya jamii na michakato yote ya kufanya maamuzi.

- **Kujenga uwezo na uelewa** wa makundi muhimu yanayogusa haki za watoto ndani katika jamii lengwa ili kuanzisha miundo na sera zenye kuwezesha ushiriki wenye maana wa watoto na vijana.

- **Kuimairisha uwezo** wa serikali za mitaa ndani ya eneo la mradi na wadau wengine katika kutengeneza sera na kutoa huduma zenye kutimiza wajibu wa serikali katika kukuza na kulinda haki za watoto na vijana na kuendeleza usawa wa kijinsia.

- **Kuboresha kutandaa pamoja** kwa wadau wa maswala ya haki za watoto ili kushirikishana visa mafunzo vinavyoweza kusaidia kuelimisha zaidi masuala ya haki za watoto na vijana na kukuza usawa wa jinsia.

Shughuli/kazi Katika ngazi ya jamii

- Mafunzo kwa makundi ya ngazi ya jamii yanayojishughulisha au kuguswa na masuala ya haki za watoto.

- Juhudi za uhamasishaji zinazotokana na Watoto na vijana.
- Makundi ya vijana katika jamii kuitisha vikao na watendaji katika jamii na wenye kufanya maamuzi ili kujadili masuala ya watoto na vijana, mambo waliyojifunza, na kuja na makubaliano juu ya utendaji wa pamoja.
- Warsha zinazohusu kupanga na kutathmini katika kila jamii zitafuatilia utekelezaji wa mradi na kutambua marekebisho ya msingi.

Wanawake na makundi ya pembezoni wakidai kuwa haki yao ya msingi kushiriki kikamilifu katika maamuzi yote ktk familia na jamii

Idadi ya Wanajamii waliweza kuelezea uzoefu wa katika kutoshiriki vema kwenye maamuzi na unyanyasaji uliokithiri unadumaza maendeleo yao.

Mnamo tarehe 12/03/2015 wanajamiii 185 ambao ni wanaume, wanawake na watoto wa rika zote walijumuika katika Kata ya Biriri, wilaya ya SIHA mkoani Kilimanjaro. Walikuja pamoja kupata taarifa ya zoezi la Tathmini ya Awali ambayo iliandaliwa na Shirika la Equitas kwa kushirikiana na TUSONGE na viongozi wa jamii kutoka Kata tatu ambazo zoezi hili lilifanyika miezi iliyopita. Stadi hii imetoa mwanga wa matatizo/magumu ambayo baadhi ya wanajamii wanapitia hasa wanawake, vijana, watoto, na waishio na ulemavu hasa katika kushikiri kikamilifu katika michakato ya maamuzi ndani ya jamii. Pia Stadi hii imetoa matokeo yahayo matatizo ambayo ni kutengwa, umaskini, unyanyasaji na kubaguliwa.

Jamii ilionyesha mwamko mkubwa kwa mradi na shauku ya kuangalia mabango ambayo yana matokeo ya Stadi ya awali na yalibandikwa katika kuta za Ofisi ya Kata. Mahojiano yalifanyika kwa zaidi ya lisaa limoja chini ya kivuli cha mti wa Acacia. Idadi kubwa ya wanajamii waliweza kuelezea uzoefu katika kutengwa, unyanyasaji na kuonyesha uhitaji wa kufanyia kazi haya matatizo. Ushiriki wa viongozi wa jamii kwa kushirikiana na Tusonge, Equitas na wa na jamii katika kukuza maadili ya haki za binadamu pia uligusiwa. Na pia waliendelea kujibu matatizo yawapatayo wanajamii. Safari ni ndefu, ila ushiriki na kushirikishwa kwa wanajamii wa Biriri ni wa kipekee na tuna mtazamo chanya kwa miradi ya baadae.
Vile vile jamii nyingine ambazo zimeshafikiwa katika utoaji wa taarifa ni Rauya – Msaranga mnamo tarehe 02/04/2015 na Ivaeny tarehe 08/04/2015 ambapo zimeonyesha utayari na mwamko mkubwa wa kushiriki katika mradi huu. Idadi ya walioshiriki Ivaeny ni 99 na Rauya ni 74. Pia wameona umuhimu wa mradi katika kutatua matatizo yanayowapata hasa wanawake, vijana, watoto, wanaoishi na ulemavu na hata wanaume pia walisema kuhusu kupigwa ambapo ni unyanyasaji wa kijinsia. Pia jamii zote ziliweza kusema ripoti ya stadi ya awali ni ya kweli na imegusa matatizo yanayowakumba katika jamii zao hasa swala zima la kuwa na ushiriki wenye tija katika ngazi za maamuzi. Kwamfano:

Nancy Mark Shirima: Mwanafunzi wa Sekondari
Anasema "Mfumodume "upo, wanawake kuteseka kwa ajili ya familia zao. Kijana ndani ya familia hashirikishwi katika kuchangia shughuli za maendeleo. Wakina baba pesa wanazo na hawataki kuzitoa kwa matumizi ya familia hawataki kujua wajibu wao. Mikopo mingi imeonekananikwa kina mama walio wengi. Nini kifanyike kutokomeza kabisa mfumodume? Vijana wapewe elimu kwa njia gani ili waweze kutoka kwenye ulevi, madawa ya kulewya, ubakaji n.k

Mr Adam Mtwenge: Diwani wa Kata ya Msaranga
Alishukuru Shirika la Tusonge kwa kuweza kufika eneo lao na kushirikiana na jamii katika kutatua matatizo yaliyomo. Alikiri kuwa mradi wa haki za binadamu ni wa muhimu sana kwenye jamii husika na kuwa utasaidia jamii kuweza kuhamasika na kushiriki katika vikao vya mitaa na kuweza kuongea bila uwoga kuhusu matatizo. Aliwasisitizia wanajamii watumie fursa zilizomo vizuri ili waweze kusikika na kuwa na ushiriki kamilifu katika ngazi za maamuzi na mradi huu.

Mwl. Emily Steven Temba - Ivaenyi
Alishauri kuwa tusiwaite watoto wa mtaani bali waitwe watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi Kata ya Ivaeny ukatili kwa kina mama (mfumo) dume upo kwa sehemu kubwa na hawana uelewa wa sehemu ipi ya kuweza kuwasaidia kielimu kuondokana na shida zao. Walemavu wapo na njia za kuwasaidia ni ngumu kwa sasa TUSONGE imewafungua masikio wanatafuta njia za kupambana kuweza kuwatafutia watoto wenye ulemavu wa aina zote njia za kuwasaidia.

MAY 2015
TUSONGE ilianza utekelezaji wa huu mradi rasmi katika jamii kwa kutoa mafunzo ya Elimu ya Haki za Binadamu kwa washiriki 24 watakaokuwa chachu ya mabadiliko katika jamii zao kwa kutumia mfumo shirikishi ili kujenga itikadi ya kulinda haki za makundi ya pembezoni.

MALENGO YA BAADAYE
- Tusonge ina m pango wa kujenga uwezo kwa jamii ipate kugundua fursa mbalimbali zilizopo, kwa mfano kuunganisha biashara zinazofanana na kisha kuwa na elimu ya pamoja kwa njia ya kushirikishana mawazo na uzoefu walionao kwa pamoja ili kutatua baadhi ya changamoto wanazokutana nazo katika biashara.
- Kuferejisha Elimu ya Haki za Binadamu kuhimiza jamii kuishi maadili yanayotunza na kukemea unyanyasaji wowote.
- Kuongeza nguvu zaidi katika masuala ya watoto.

JITIHADA ZA TUSONGE ZIMEWEZESHWA NA MSAADA KUTOKA KWA WABIA WETU:

- **Wafadhili wa Mradi wa TUSONGE Mkate kwa Dunia (Bread for the World Development Ujerumani)**
- **Kituo cha haki za binadamu Equitas-Canada**